

Kanuni za Kifonolojia za Uingizaji wa Vinyambuo Vitenzi katika Kamusi: Mifano kutoka Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013)

Fatuma Abdallah

Baraza la Kiswahili la Taifa, Tanzania

Ikisiri

Utungaji kamusi ni kazi ya kisayansi ambayo mbali na mambo mengine inahusisha matawi mbalimbali ya isimu. Katika kuisitiza suala hili, Mdee (2010) anaeleza kwamba mwanaleksikografia anawajibika kufahamu japo kwa uchache maarifa ya nyanja za isimu ili yamsaidie katika kueleza leksimu anazoziteua na kuziingiza katika kamusi. Maelezo haya yanadhihirisha kwamba ni muhimu maarifa ya nyanja mbalimbali za isimu yakazingatiwa wakati wa kuingiza vidahizo na taarifa katika kamusi ikiwamo vinyambuo vitenzi. Makala haya yanalenga kufafanua kanuni za kifonolojia zilizingatiwa wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la tatu (kuanzia sasa KKS 3). Pia makala haya yanaeleza athari za kutokufuata kanuni hizo na itatoa mapendekezo ya nini kifanyike ili uingizaji wa vinyambuo vitenzi uwe wa ufanisi zaidi katika kamusi mbalimbali za Kiswahili ikiwa ni pamoja na Kiswahili Sanifu.

Maneno Muhimu: Fonolojia, kanuni, vitenzi, Kamusi.

Utangulizi

Fonolojia ni tawi la isimu linalochunguza mfumo wa sauti katika lugha fulani mahususi. Massamba na wenzake (2013) wanaeleza kwamba fonolojia hujishughulisha na vipengele mbalimbali ambavyo ni kama vile matamshi, mkazo, lafudhi, mfuatano wa sauti katika kuunda silabi, mfuatano wa sauti katika kuunda mofimu, mfuatano wa mofimu katika kuunda maneno na othografia. Katika makala haya, kanuni za fonolojia zilizoshughulikiwa ni zile zinazohusiana na mfuatano wa sauti/ mofimu katika kuunda maneno. Kanuni hizi zisipozingatiwa wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi husababisha vinyambuo vitenzi vinavyoingizwa katika kamusi visiwe sahihi.

Kanuni za Kifonolojia Zilizozingatiwa wakati wa Uingizaji wa Vinyambuo Vitenzi katika KKS 3

Katika sehemu hii tumefafanua kanuni za kifonolojia zilizotumika wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika KKS 3. Kwa ujumla, uingizaji wa vinyambuo vitenzi katika KKS 3 ulitawaliwa na kanuni mbili za kifonolojia. Kanuni hizo ni tangamano la irabu na udondoshaji/upachikaji.

Tangamano la Irabu

Huu ni mchakato wa kifonolojia unaozihusu irabu zilizo jirani ambapo athari ya irabu moja kwenye irabu nyingine huzifanya irabu hizo zielekee kufanana kabisa au kufanana kiasi katika sifa zake za matamshi. Mgullu (2005) anaeleza kwamba tangamano la irabu ni utratibu wa irabu fulani kukubali kuandamna katika mazinira maalumu. Kwa upande wa Massamba na wenzake (2013) wanaeleza kwamba tangamano la irabu linahusu mabadiliko ya sauti yanayosababishwa na hali ya utangamano inayojitokeza katika baadhi ya vitamkwa ambapo kuna kuwa na namna fulani ya kufanana au kukubaliana kwa vitamkwa vilivyo jirani. Mchakato huu huzihusu irabu /u, a na i/ na irabu /ɔ na ε/. Irabu /u na i/ ni za juu, irabu /ɔ na ε/ ni za kati na irabu /a/ ni ya chini. Katika kanuni hii ikiwa mzizi wa neno la msingi linalotumika kuunda kinyambuo kitenzi una irabu /u/, /a/, au /i/ kiambishi kinachowakilisha dhana ya kinyambuo kitenzi kinalazimika kuwa na irabu /i/ na ikiwa mzizi wa neno la msingi una irabu /ɔ na ε/ kiambishi kinachowakilisha dhana ya kinyambuo kitenzi kinalazimika kuwa na irabu /ε/.

Kanuni hii imetumika katika kuunda vinyambuo vitenzi vyenye dhana ya utendea, utendeka, utendesha na utendewa vilivyoingizwa katika KKS 3 kama kidahizo kikuu au kidahizo mfuto. Jedwali linalofuata linaonesha namna kanuni ya tangamano la irabu ilivyotumika katika baadhi ya vinyambuo vitenzi vilivyoingizwa katika KKS 3.

Jedwali la 1: Vinyambuo Vitenzi Vilivyotumia Kanuni ya Tangamano la Irabu

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Vinyambuo Vitenzi			
			Utendea	Utendeka	Utendesha	Utendewa
i.	imba	imb-	imbia	imbika	imbisha	mbiwa
ii.	tunga	tung-	tungia	tungika	tungisha	tungiwa
iii.	panga	pang-	pangia	pangika	pangisha	pangiwa
iv.	cheza	chez-	chezea	chezeka	chezsha	chezewa
v.	omba	omb-	ombea	ombeka	ombesha	ombewa
vi.	oa	o-	olea	oleka	olesha	olewa
vii.	sia	si-	silia	silika	silisha	siliwa

Chanzo: KKS 3

Kama inavyoonekana katika jedwali la 1 hapo juu, kanuni ya tangamano la irabu imetumika katika kuunda vinyambuo vitenzi vilivyoingizwa katika KKS 3.

Katika jedwali hapo juu ni dhahiri kwamba viambishi vya dhana ya utendea, utendeka, utendesha na utendewa vinabadilikabadilika. Kubadilikabadilika kwa viambishi hivyo kunasababishwa na irabu iliyo katika mzizi wa kitenzi. Tutazame ufafanuzi zaidi wa namna kanuni ya tangamano la irabu ilivyozingatiwa wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi kwenye KKS 3 katika sehemu inayofuata.

Utendea

Mgullu (2005) anaeleza utendea kama ni kauli inayotumiwa kueleza hali ya mtendaji kutenda jambo fulani pakiwa na ala inayotumika kutendea jambo, mahali panapotandekwa jambo, sababu ya kutendeka jambo, mwelekeo wa tendo na tendo kufanyika kwa niamba. Kwa upande wa dhana ya utendea viambishi vinavyowakilisha dhana hii ni *-i-*, *-e-*, *-le-*, na *-li-*. Viambishi hivyo vinajitokeza kwa kutegemea kanuni ya tangamano la irabu kama ifuatavyo:

- i. Kiambishi *-i-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /u, a au i/.
- ii. kiambishi *-e-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /ɔ au ε/.
- iii. Kiambishi *-li-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /u, a au i/.
- iv. Kiambishi *-le-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /ɔ na ε/. Data katika jedwali la 2 inafafanua zaidi kanunihii

Jedwali la 2: Vinyambuo Vitenzi vya Utendea Vilivyondwa kwa Kanuni ya Tangamano la Irabu

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Kiambishi cha Utendea	Kinyambuo Kitenzi
i.	fata	fat-	-i-	fatia
ii.	imba	imb-	-i-	imbia
iii.	punja	punj-	-i-	punjia
iv.	sema	sem-	-e-	semea
v.	choma	chom-	-e-	chomea
vi	vaa	va-	-li-	valia
vii	vua	vu-	-li-	vulia
viii.	lia	li-	-li-	lilia
ix.	lea	le-	-le-	lelea
x.	oa	o-	-le-	olea

Chanzo: KKS 3

Utendeka

Utendeka ni dhana inayoeleza jambo ambalo limetendeka. Utendeka hautilii maanani mtenda jambo bali kutendeka kwa jambo (Mgullu 2005). Dhana ya utendeka inawakilishwa na viambishi *-ik-*, *-ek-*, *-lek-*, na *-lik-*. Viambishi hivyo vimepachikwa kwa kutegemea kanuni ya tangamano la irabu kama ifuatavyo:

- i. Kiambishi *-ik-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /u, a au i/.
- ii. Kiambishi *-ek-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /ɔ na ε/.
- iii. Kiambishi *-lik-* itajitokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /u, a au i/.
- iv. Kiambishi *-lek-* kitajitokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /ɔ na ε/. Data katika jedwali la 3 fafanua zaidi kanuni hizi.

Jedwali la 3: Vinyambuo Vitenzi vya Utendeka Vilivyoundwa kwa Kanuni ya Tangamano la irabu

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Kiambishi Utendeka	cha	Kinyambuo Kitenzi
i.	panga	pang-	-ik-		pangika
ii.	imba	imb-	-ik-		imbika
iii.	funga	fung-	-ik-		fungika
iv.	sema	sem-	-ek-		semeka
v.	omba	omb-	-ek-		ombeka
vi.	vaa	va-	-lik-		valika
vii.	vua	vu-	-lik-		vulika
viii.	tia	ti-	-lik-		tilika
ix.	lea	le-	-lek-		leleka
x.	oa	o-	-lek-		oleka

Chanzo: KKS 3

Utendesha

Utendesha ni dhana yenye uhusika wa aina mbili mosi, mtu anayefanya mtu au watu wengine wafanye jambo fulani ambapo si lazima mtu huyo afanye jambo hilo na pili mtu au watu wanaofanywa wafanye jambo fulani na mtu mwingine. Mtu au watu hawa lazima watende jambo hilo (Mgullu 2005). Dhana ya utendesha inawakilishwa na viambishi *-ish-*, *-esh-*, *-lesh-*, na *-lish-*. Viambishi hivyo vimepachikwa kwa kutegemea kanuni ya tangamano la irabu kama ifuatavyo:

- i. Kiambishi *-ish-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /u, a au i/.
- ii. Kiambishi *-esh-* kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /ɔ na ε/.

- iii. Kiambishi **-lish-** linajitokeza ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /u, a au i/.
- iv. Kiambishi **-lesh-** kinajitokeza ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /ɔ na ε/. Data katika jedwali la 4 inafafanua zaidi kanuni hizo.

Jedwali la 4: Vinyambuo Vitenzi vya Utendesha Vilivyoundwa kwa Kanuni ya Tangamano la irabu

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Kiambishi cha Utendesha	Kinyambuo Kitenzi
i.	panga	pang-	-ish-	pangisha
ii.	fika	fik-	-ish-	fikisha
iii.	punga	pung-	-ish-	pungisha
iv.	pweta	pwet-	-esh-	pwetesh
v.	soma	som-	-esh-	somesha
vi.	kaa	ka-	-lish-	kalisha
vii.	fua	fu-	-lish-	fulisha
viii.	tia	ti-	-lish-	tilisha
ix.	pea	pe-	-lesh-	pelesha
x.	ng'oa	ng'o-	-lesh-	ng'olesha

Chanzo: KKS 3

Utendewa

Dhana hii hutumika kuelezea hali ya mtu kufanyiwa jambo fulani na mtu mwingine. Dhana ya utendewa inawakilishwa na viambishi *-iw-*, *-ew-*, *-lew-*, na *-liw-*. Mgullu (2005) anafafanua kwamba utendewa hueleza yupo mtu au watu wanaofanya jambo kwa niaba ya mtu au watu wengine na kwamba wanaotendewa ndio hunufaika na kuapata asara kutokan ana jambo lililotendwa. Viambishi hivyo vimepachikwa kwa kutegemea kanuni ya tangamano la irabu kama ifuatavyo:

- i. Kiambishi **-iw-** kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /u, a na i/.
- ii. Kiambishi **-ew-** kinatokea ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na konsonanti na una irabu /ɔ na ε/.
- iii. Kiambishi **-liw-** kinajitokeza ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /u, a au i/.
- iv. Kiambishi **-lew-** kinajitokeza ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na irabu /ɔ na ε/. Data katika jedwali la 5 inadhihirisha hoja hii:

Jedwali la 5: Vinyambuo Vitenzi vya Utendewa Vilivyoundwa kwa Kanuni ya Tangamano la Irabu

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Kiambishi cha Utendewa	Kinyambuo Kitenzi
i.	pika	pik-	-iw-	pikiwa
ii.	imba	imb-	-iw-	imbiwa
iii.	umba	umb-	-iw-	umbiwa
iv.	cheza	chez-	-ew-	chezewa
v.	soma	som-	-ew-	somewa
vi	kaa	ka-	-liw-	kaliwa
vii	fua	fu-	-liw-	fuliwa
viii.	tia	ti-	-liw-	tiliwa
ix.	pea	pe-	-lew-	pelewa
x.	zoa	zo-	-lew-	zolewa

Chanzo: KKS 3

Kutokana na data na maelezo yaliyotolewa hapo juu ni dhahiri kwamba irabu ya mzizi katika data hizo inaathiri utokeaji wa irabu za vinyambuo vitenzi vya utendea, utendeka, utendesha na utendwa na kwamba kanuni hiyo isipofuatwa vinyambuo vitenzi hivyo havitakuwa sahihi. Imedhihirika kwamba ikiwa irabu ya mzizi ni /u/, /a/, au /i/ kiambishi cha kinyambuo kitenzi kinalazimika kuwa na irabu /i/ na ikiwa mzizi wa neno la msingi una irabu /ɔ/ na /ɛ/ kiambishi cha kinyambuo kitenzi kinalazimika kuwa na irabu /ɛ/.

Udondoshaji na Upachikaji wa Sauti

Upachikaji wa viambishi hivi katika mizizi ya maneno ili kuunda vinyambuo vitenzi hufanyika kwa kuzingatia kanuni maalumu zinazohusiana na unyambulishaji. Kiango (2008) anaeleza kwamba michakato yote ya unyambulishaji hutawaliwa na kanuni za kifonolojia na kimofolojia. Hivyo, ni dhahiri kwamba uingizaji wa vinyambuo vitenzi katika kamusi unapaswa pia kuzingatia kanuni za kifonolojia na kimofolojia. Hata hivyo, kanuni za kifonolojia zinazotumika katika kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi ni kipengele ambacho hakijafanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa.

Udondoshaji na upachikaji ni kanuni inayohusu kuongezwa na kuachwa kwa sauti fulani wakati sauti au mofimu mbili zinapokaribiana ili kuunda maneno. Kanuni hii imetumika ambapo wakati wa kupachika viambishi nyambulishi vinavyotumika kuunda vinyambuo vitenzi vilivyoingizwa katika KKS 3. Kanuni ya udondoshaji na upachikaji imejitokeza kwa namna mbili. Mosi, kanuni hii imetumika katika maneno huru yanayotoka katika lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kiajemi na Kiarabu. Pili, kanuni hii imetumika katika maneno ya msingi yenye mzizi unaoishia na sauti /k/ yaliyotumika kuunda vinyambuo vitenzi vya utendesha.

Kanuni ya Upachikaji na Udondoshaji katika Maneno ya Mkopo

Wakati wa uingizaji wa vinyambuo vitenzi katika KKS 3 upachikaji na udondoshaji umetumika katika vitenzi vya mkopo ambapo irabu ishilizi /i/ na u/ ambazo huwa mwishoni mwa maneno ya mkopo zimedondoshwa katika mazingira tofautitofauti. Udondoshaji umefanyika baada ya upachikaji wa viambishi nyambulishi katika shina la kitenzi. Vilevile, irabu ishilizi /a/ imepachikwa katika vinyambuo vitenzi mara tu baada ya kupachika viambishi nyambulishi. Upachikaji wa irabu ishilizi /a/ katika vitenzi vya mkopo unavifanya vitenzi hivyo viwe na ruwaza ya vitenzi vya Kiswahili ambavyo huishia na irabu /a/. Data katika jedwali la 6 inaonyesha namna kanuni ya udondoshaji na upachikaji ilivyotumika wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi vinavyotokana na maneno ya mkopo katika KKS 3.

Jedwali la 6: Kanuni ya Upachikaji na Udondoshaji kwa Vitenzi vya Mkopo

Na.	Kitenzi	Etimolojia	Kinyambuo Kitenzi
i.	rapu	Kiingereza	rapia, rapika, rapisha
ii.	faini	Kiingereza	fainia, fainiana, fainika, fainisha, fainiwa
iii.	ramisi	Kiajemi	ramisia, ramisika, ramisisha
iv.	busu	Kiajemi	busia, busiana, busika, busisha, busiwa
v.	dhoofu	Kiarabu	dhoofia, dhoofika, dhoofisha
vi.	rudufu	Kiarabu	rudufia, rudufika, rudufisha, rudufiwa
vii.	rudi	Kiarabu	rudia, rudika, rudisha, rudiwa
viii.	kodi	Kihindi	kodia, kodiana, kodika, kodisha, kodiwa.

Chanzo: KKS 3

Katika jedwali la 6 hapo juu inaonekana dhahiri kwamba kuna udondoshaji wa irabu /i/ na u/ ambazo zipo mwishoni mwa vitenzi vya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza, Kiajemi, Kiarabu na Kihindi. Vilevile kuna upachikaji wa irabu /a/ ambayo ni kiambishi tamati kinachokamilisha maana ya kitenzi na pia kufanya kinyambuo kitenzi kinachohusika kuwa na ruwaza ya vitenzi vya Kiswahili. Tutazame ufafanuzi zaidi wa kanuni ya udondoshaji katika sehemu inayofuata.

Kanuni ya Udondoshaji wa irabu /i/

Irabu /i/ imedondoshwa kutokana na kufuatwa na irabu inayofanana nayo ya kiambishi nyambulishi. Jedwali la 7 linaonyesha namna kanuni ya udondoshaji ilivyotumika wakati wa upachikaji wa viambishi nyambulishi ili kuunda vinyambuo vitenzi vilivyoingizwa katika KKS 3.

Jedwali la 7: Vinyambuo Vitenzi Vilivyotokana na Kanuni ya Udondoshaji wa Irabu /i/

Na.	Kitenzi	Kiambishi Nyambulishi	Kinyambuo Kitenzi kabla ya Udondoshaji	Kinyambuo Kitenzi baada ya Udondoshaji
i.	faini	-i-, -ian-, -ik-, -ish-, -iw-	fainiia, fainiiana, fainiika, fainiisha, fainiwa-	fainia, fainiana, fainika, fainisha, fainiwa
ii.	ramisi	-i-, ik-, -ish-,	ramisiia, ramisiika, ramisiisha	ramisia, ramisika, ramisisha
iii.	rudi	-i-, ik-, -ish-, -iw-	rudiia, rudiika, rudiisha, rudiwa	rudia, rudika, ruisha, rudiwa
iv.	kodi	-i-, -ian-, -ik-, -ish-, -iw-	kodiia, kodiiana, kodika, kodiisha, kodiwa.	kodia, kodiana, kodika, kodisha, kodiwa.

Chanzo: KKS 3

Katika jedwali la 7 hapo juu, kanuni ya udondoshaji imetumika wakati wa kuambika viambishi nyambulishi katika vitenzi huru vinavyotoka lugha za kigeni vinavyoishia na irabu /i/. Kwa kuwa vitenzi hivyo ni huru na vinaishia na irabu /i/ vinapoambikwa viambishi nyambulishi vinavyoanza na irabu /i/ irabu ya mwishoni mwa kitenzi hudondoka. Kwa mfano, katika jedwali la 7 kitenzi *kodi* kimeambikwa viambishi *-i, -ian- -ik, -ish-* na *-iw-* kuunda vinyambuo vitenzi *kodiia, kodiiana, kodiika, kodiisha*, na *kodiwa*. Katika vinyambuo vitenzi hivi kuna irabu /i/ ya mwishoni mwa kitenzi na irabu /i/ ya kiambishi nyambulishi zimefuatana. Irabu /i/ ya mwishoni mwa kitenzi imedondoshwa ili kuunda vinyambuo vitenzi *kodia, kodiana, kodika, kodisha, kodiwa*.

Kanuni ya Undoshaji wa Irabu /u/

Irabu /u/ imedondoshwa kutokana na kufuatiwa na irabu /i/ inayofanana nayo katika mahala pa matamshi. Irabu /i/ na /u/ zote ni irabu za juu. Hivyo, katika kuunda vinyambuo vitenzi irabu /u/ iliyo mwishoni mwa kitenzi kinachohusika hudondoshwa. Jedwali la 8 linaonesha udondoshaji wa irabu /u/ wakati wa kuunda vinyambuo vitenzi vinavyoingizwa katika KKS 3.

Jedwali la 8: Vinyambuo Vitenzi vilivyotokana na Kanuni ya Udondoshaji wa Irabu /u/

Na.	Kitenzi	Kiambishi Nyambulishi	Kinyambuo Kitenzi kabla ya Udondoshaji	Kinyambuo Kitenzi baada ya Udondoshaji
ii.	busu	-i-, ik-, -ish-,	busuia, busuiana, busuika, busuisha, busuiwa	busia, busiana, busika, busisha, busiwa
iii.	dhoofu	-i-, ik-, -ish-,	dhoofuia, dhoofuika, dhoofuisha.	dhoofia, dhoofika, dhoofisha.
iii.	tubu	-i-, -ik-, -ish-, -iw-	tubuia, tubuika, tubuisha, tubuiwa	tubia, tubika, tubisha, tubiwa

Chanzo: KKS 3

Katika jedwali la 8, kanuni ya udondoshaji imejitokeza wakati wa kuambika viambishi nyambulishi katika vitenzi huru vinavyotokana na lugha za kigeni vinavyoishia na irabu /u/. Kwa kuwa vitenzi hivyo ni huru na vinaishia na irabu /u/ vinapoambikwa viambishi nyambulishi vinavyoanza na irabu /i/ inayofanana mahali pa matamshi na irabu /u/, irabu /u/ ya mwishoni mwa kitenzi hudondoshwa. Matalani, katika jedwali la 8 kitenzi *busu* kimeambikwa viambishi *-ia*, *-ik-*, na *-ish-* kuunda vinyambuo vitenzi *busuia*, *busuika*, na *busuisha*. Katika vinyambuo vitenzi hivi kuna irabu /u/ ya mwishoni mwa kitenzi na irabu /i/ ya kiambishi nyambulishi zote za juu zimefuatana. Irabu /u/ ya mwishoni mwa kitenzi imedondoshwa ili kuunda vinyambuo vitenzi *busia*, *busika*, na *busisha*.

Kutokana na data katika jedwali la 7 na 8, ni dhahiri kwamba mchakato wa udondoshaji ni muhimu kuzingatiwa wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi. Mchakato huu usipozingatiwa utasababisha kuunda vinyambuo vitenzi visivyo sahihi na visivyo katika matumizi.

Wesana-Chomi (2003) akifafanua kuhusu mabadiliko ya viambishi tamati vya maneno ya mkopo wakati wa upachikaji wa viambishi nyambulishi katika vitenzi ili kuunda vinyambuo vitenzi anaeleza kwamba kutokana na usawazisho wa matamshi irabu ya mwishoni mwa mzizi ya maneno ya mkopo humezwa na irabu ya kwanza ya kiambishi nyambulishi. Tunakubaliana naye kuhusiana na kusawazisa matamshi ingawa hakueleza ni kwa vipi irabu hiyo inamezwa. Kwa maoni yetu irabu ya mwishoni mwa maneno ya mkopo hudondoshwa wakati wa upachikaji wa viambishi nyambulishi.

Udondoshaji wa Sauti /k/ na irabu ya Kiambishi cha Utendesha

Kanuni ya udondoshaji imetumika katika kuunda vinyambuo vitenzi vyenye kuwakilisha dhana ya utendesha ambavyo mzizi wa neno la msingi unaishia na

sauti /k/. Ikiwa mzizi wa neno la msingi unaishia na sauti /k/, ili kuunda kinyambuo kitenzi sahihi sauti /k/ ya kwenye mzizi wa neno la msingi na irabu ya mwanzo ya kiambishi cha utendesha hudondoshwa. Jedwali la 9 linaonesha namna kanuni ya udondoshaji ilivyozingatiwa katika kuingiza vinyambuo vitenzi katika KKS 3.

Jedwali la 9: Kanuni ya Udondoshaji wa sauti /k/ na irabu ya Kiambishi Utendesha

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Kiambishi Nyambulishi	Kinyambuo Kitenzi Kisichosahihi	Kinyambuo Kitenzi Sahihi
i.	pumzika	pumzik-	-ish-	pumzikisha	pumzisha
ii.	potoka	potok-	-esh-	potokesha	potosha
iii.	ruka	ruk-	-ish-	rukisha	rusha
iv.	teremka	teremk-	-ish-	teremkisha	teremsha
v.	zeeka	zeek-	-esh-	zeekesha	zeesha

Chanzo: KKS 3

Jedwali la 9 hapo juu linaonyesha namna sauti /k/ katika mzizi wa neno la msingi na irabu ya mwanzo ya kiambishi nyambulishi ilivyodondoshwa ili kuunda vinyambuo vitenzi vya utendesha. Katika mazingira kama hayo kiambishi cha utendesha hakiwezi kuambikwa katika mzizi wa neno la msingi unaoishia na konsonanti /k/ bila kufanyiwa mabadiliko ya kifonolojia ya kutumia kanuni ya udondoshaji. Kwa mfano si sahihi kuwa na maneno kama vile zeekesha, teremkisha, potokesha bali maneno zeesha, teremsha na potosha baada ya kufuata kanuni ya udondoshaji wa sauti /k/ na irabu ya mwanzao ya kiambishi nyambulishi cha utendesha.

Athari za kutofuata kanuni za kifonolojia wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi

Kwa ujumla, athari inayotokana na kutokufuata kanuni za kifonolojia wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi ni kuingiza maneno yasiyo sahihi. Kuingiza maneno yasiyo sahihi kunamaanisha kwamba maneno hayo hayapo katika matumizi jambo ambalo ni kosa kileksikografia. Massamba (2012) anafafanua kwamba fonolojia hujishughulisha na jinsi sauti za lugha zinavyotumika katika kuunda maneno ambayo huwakilisha maana. Ikiwa kanuni hazikufuatwa maana yake ni kwamba maneno yatakayoundwa hayatakuwa na maana na pia hayatakuwa katika matumizi. Mdee (2010) anaeleza kwamba dhima ya leksikografia ni kunukuu matumizi ya lugha kama yanavyojidhihirisha katika mazungumzo au maandishi. Hivyo basi, ikiwa maneno yatakayoingizwa katika kamusi katika ayapo katika matumizi yaani katika mazungumzo na maandishi ni kosa kileksikografia.

Miongoni mwa kanuni ambazo hazikufuatwa ni kanuni ya tangamano la irabu. Kutokufuata kanuni hii kulibainika katika baadhi ya vinyambuo vitenzi ambavyo vimeingizwa katika KKS 3 kama vidahizo mfuto. Kwa mfano, kitenzi sogeza kimeambikwa viambishi *-i-*, *-ian-* na *-ik-* kuunda vinyambuo vitenzi *sogezia*, *sogeziana* na *sogezika*. Vinyambuo vitenzi hivyo si sahihi kwa kuwa upachikaji wa viambishi nyambulishi haukufuata kanuni ya tangamano la irabu. Vitenzi *sogezia*, *sogeziana* na *sogezika* havipo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili hivyo ni makosa kuviingiza katika kamusi. Kulingana na kanuni ya tangamano la irabu kwa kuwa mzizi *sogez-* wa neno *sogeza* una irabu ya kati yaani /ε au ɔ/ kinyambo kitenzi kilipaswa kumbikwa viambishi *-e-*, *ean-* na *-ek-* kuunda vinyambuo vitenzi *sogezea*, *zozezeana* na *sogezeka*.

Wakati wa uingizaji wa vinyambuo vitenzi katika KKS 3 kanuni ya udondoshaji wa sauti /k/ ya mwishoni mwa mzizi wa maneno yanayoishia na sauti /k/ na irabu ya mwanzo ya kiambishi cha utendesha haikufuatwa. Data katika jedwali la 10 inadhahirisha vinyambuo vitenzi vilivyoingizwa kwa makosa katika KKS 3 kutokana na kuambatisha kiambishi cha utendesha kwenye neno la msingi ambalo mzizi wake unaishia na konsonanti /k/.

Jedwali la 10: Vinyambuo Vitenzi vya Utendesha Vilivyokiuka Kanuni ya Udondoshaji

Na.	Neno la Msingi	Mzizi	Kiambishi Nyambulishi	Kinyambuo Kitenzi Kisichosahihi	Kinyambuo Kitenzi Sahihi
i.	babaikika	babaikik-	-ish-	babai/isha	babaisha
ii.	chachuka	chachuk-	-ish-	chachu/isha	chachusha
iii.	faidika	faidik-	-ish-	faidik/isha	faidisha
iv.	potoka	potok-	-esh-	potok/esha	potosha
v.	tweka	twek-	-esh-	twek/esha	twesha

Chanzo: KKS 3

Katika jedwali la 10 hapo juu, vinyambuo vitenzi visivyo sahihi vimeingizwa katika kamusi kama vidahizo mfuto. Katika data hiyo ili kuunda kinyambuo kitenzi chenye dhana ya utendesha kilicho sahihi kwa maneno ya msingi yenye mzizi unaoishia na konsonanti /k/ udondoshaji wa sauti mbili hauna budi kufanyika. Sauti hizo ni konsonanti /k/ mwishoni mwa mzizi na irabu ya kiambishi cha utendesha ambayo inaifuatia konsonanti hiyo. Safu ya mwisho kulia katika jedwali la 10 hapo juu inaonesha vinyambuo vitenzi sahihi baada ya udondoshaji wa sauti kufanyika. Sauti hizo ni konsonanti /k/ ya mwishoni mwa mzizi wa kitenzi na irabu /i na ε/ ambazo ni irabu za mwanzoni mwa kiambishi cha utendesha zinazofuata mara tu baada ya konsonanti /k/ iliyo mwishoni mwa mzizi wa neno la msingi.

Kutokana na data hapo juu ni dhahiri kwamba ni muhimu kuzingatia kanuni za kifonolojia wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi. Kufanya hivi kutasaidia watunga kamusi kutokuingiza maneno yasiyotumika katika kamusi. Mdee (1995) anaeleza kwamba ni makosa kuingiza katika kamusi maneno ambayo hajawai kutumiwa na wazungumzaji wa lugha. Tunaunga mkono hoja hii ya Mdee kwa kuwa si rahisi kwa mtumiaji wa kamusi kutafuta neno ambalo halijawahi kutumika na halipo kabisa katika matumizi. Pia, kuiniza maneno yasiyotumika katika kamusi kunachangia kuongeza gharama ya uandaaji wa kamusi jambo linaloathiri pia bei ya kamusi.

Tunatambua kwamba baadhi ya vinyambuo vitenzi vinaonekana kuwa sahihi kimuundo lakini kisemantiki havina maana na havitumiki kabisa katika mawasiliano ya wanajamii. Maoni yetu ni kwamba vinyambuo vya namna hii vishughulikiwe katika vitabu vya sarufi na siyo katika kamusi. Hii ni kwa sababu kamusi hufafanua maneno kwa muhtasari ilihali vitabu vya sarufi vinafafanu maneno na kanuni kwa kina na hivyo kuweza kutoa maelezo toshelevu.

Hitimisho

Ni muhimu watunga kamusi kuzingatia kanuni za kifonolijia miongoni mwa nyingine wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika kamusi. Kufanya hivi kutawasaidia watumiaji wa kamusi kupata taarifa zinazohusiana na vinyambuo vitenzi kwa usahihi. Huu pia utakuwa ni msaada kwa wajifunzaji wa lugha ambapo zana mojawapo ni kamusi hasa kamusi sanifu. Kufuata kanuni vilevile kutawasaidia watunga kamusi kuingiza vinyambuo vitenzi kwa ufasaha. Aidha, ni muhimu kwa watunga kamusi kushughulikia kila kinyambuo kitenzi na kila kiambishi kinachopachikwa katika mzizi wa neno kwa upekee wake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kila kiambishi kinapata maana kulingana na mahali/nafasi kilipotumika katika neno. Wakati wa kuingiza vinyambuo vitenzi katika KKS 3 baadhi ya kanuni hazikufuatwa kutokana na kutumia kanuni za upachikaji wa viambishi nyambulishi katika vitenzi kwa ujumlajumla. Wakati mwingine baadhi ya vitenzi vinaweza kuhitaji kutumia kanuni ambayo haitumiki katika vitenzi vingine. Kwa mazingira kama haya mtunga kamusi hawezi kukwepa kuvishughulikia vinyambuo vitenzi kwa upekee wake.

Marejeo

- Howard, J. (2003). *Lexicography: An Introduction*. New York. Tylor & Francis Routledge
- Kiango, J. G. (2006). "Uingizaji wa Vinyambuo Nomino katika Kamusi za Kiswahili" Katika *Mulika*. Dar es Salaam. TUKI. Uk. 60-77.
- Kiango (2008). "Sarufi ya Vinyambuo Vitenzi vya Kiswahili: Mitazamo mbalimbali kuhusu Kanuni za Unyambuaji". Katika *Nadharria katika Taaluma za Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Nairobi: Moi University Press. Uk. 45-58.

- Kiango, J. G. (2015). *Bantu Lexicography: A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary*. Nairobi: Oxford University Press.
- Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B., Y.M. Kihore na Y.P. Msanjila (2013). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mdee, J. S. (1994). Swahili Learners' Views on the Need for a Monolingual Swahili Pedagogical Dictionary katika <http://lexikos.journals.ac.za>. Uk. 230-248.
- Mdee, J.S. (1995). "Misingi ya Uteuzi wa Vidahizo katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu." Katika *Misingi ya Utungaji wa Kamusi: Leksikografia ya Kiswahili 2*. Uk .45-57.
- Mdee, J. S. (2010). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mgullu, R. S. (2005). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi. Longhorn Publishers.
- Wesana-Chomi (2003) *Kozi Fupi Tangulizi katika Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Sebha. Chuo Kikuu cha Sebha.

